

MAENEZI YA LUGHA YA KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI: MAFANIKIO NA CHANGAMOTO

JOHN HAMU HABWE

Utafiti huu unachunguza maenezi ya lugha ya Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini kwa kuangazia njia zilizotumika kuisambaza hii lugha ya Kiswahili nchini humo. Unachunguza pia changamoto za lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini na mustakabali wake. Data ya utafiti huu imekusanywa nyanjani kupitia kifaa cha mahojiano ambapo tuliwahoji wenyeji wa Sudan Kusini na wafanyakazi wa mashirika mbalimbali nchini Sudan Kusini. Utafiti huu umebaini kuwa Kiswahili kimeingia Sudan Kusini kwa msaada wa nyenzo mbalimbali kama vile vita, biashara, elimu, maingiliano ya mipakani, dini na ndoa. Utafiti huu pia unajadili baadhi ya vizuizi vinavyoweza kutatiza ukuaji na ueneaji wa Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini kama vile tishio kubwa la ushindani na upinzani wa makundi ya lugha za Sudan Kusini na lugha ya Kiarabu ambayo ndiyo lugha ya maenezi mapana, na hali kadhalika lugha ya Kiingereza ambayo ni moja katika lugha zinazoenziwa katika taifa la Sudan Kusini hasa kwa kuwa lugha ya kimataifa. Imebainika pia kuwa sababu kubwa za kujifundisha Kiswahili kwa wenyeji wengi wa Sudan Kusini kumechangiwa na haja ya kutaka kujitambulisha na kujinasibisha na makundi mbalimbali ya Afrika Mashariki. Utafiti huu unahoji pia kuwa mustakabali wa lugha ya Kiswahili utategemea sera ya lugha nchini Sudan Kusini na utekelezaji wa matakwa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ya kufanya Kiswahili kuwa lugha ya maenezi mapana katika eneo la Afrika Mashariki inakopatikana nchi ya Sudan Kusini.

Utangulizi

Utafiti huu unahusu maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini. Hususan unajikita katika kubaini njia zilizosaidia kueneza Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini. Kama tunavyojua tayari lugha ya Kiswahili imeenea katika mataifa mbalimbali duniani licha ya chimbuko lake kuwa pwani ya Afrika Mashariki. Njia mbalimbali zilitumika katika kukisambaza Kiswahili nje ya mipaka yake ya asili. Baadhi ya sababu hizi ni biashara, elimu, uhamaji, dini, vita na mitagusano ya mipakani. Baadhi ya maeneo ambamo Kiswahili kimeenea ni barani Afrika hali mengine yamo nje ya bara la Afrika. Baadhi ya maeneo ya Afrika ambamo Kiswahili kimeenea ni Uganda, Rwanda, Burundi, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Msumbiji, Malawi, Zambia, Visiwa vya Komoro, Ethiopia, Mayote na kwingineko. Katika mataifa ya Kiafrika Kiswahili kinatekeleza majukumu mbalimbali. Nchini Tanzania Kiswahili ni lugha rasmi na lugha ya taifa vile vile. Inatumiwa kusomesha katika shule za msingi na pia shule za sekondari. Lugha ya Kiswahili inafundishwa kama mojawapo ya taaluma katika vyuo vikuu nchini Tanzania. Tanzania pia ina taasisi ya utafiti wa Kiswahili inayojulikana kama Taasisi ya Taaluma ya Kiswahili (TATAKI). Mbali na taasisi hii Tanzania ina baraza la kushughulikia maendeleo ya Kiswahili linalojulikana kama Baraza la Kiswahili Tanzania (BAKITA). Kiswahili kinatumiwa kama lugha ya utambulisho wa kitaifa nchini Tanzania na nyenzo ya kuunganisha makabila yake. Kunayo taasisi nyingine Tanzania yenye makao yake Kisiwani Zanzibar. Taasisi hii inayojulikana kama Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA)

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

inafanya utafiti katika lugha ya Kiswahili. Nchini Kenya Kiswahili ni lugha ya taifa na lugha rasmi vile vile. Kiswahili ni somo la kutahiniwa katika shule za msingi na sekondari nchini humo. Kenya. Pia kinasomeshwa kama somo la taaluma katika vyuo vikuu vyote vya umma na baadhi ya vyuo vya kibinafsi. Nchini Kenya na Tanzania kuna makundi yapatayo kumi na nane ya wasemaji asilia wa lugha ya Kiswahili. Nchini Rwanda Kiswahili ni lugha rasmi mbali na lugha ya Kiingereza. Lugha ya Kiswahili pia inafundishwa shuleni kama somo. Nchini Burundi lugha ya Kiswahili inafundishwa katika shule za msingi. Katika nchi ya Burundi kuna maenezi ya haja ya lugha ya Kiswahili. Lugha ya Kiswahili imeoredheshwa kama moja ya lugha rasmi. Pia lugha ya Kiswahili inafundishwa kama mojawapo ya masomo katika mtaala mpya. Nchini Uganda Kiswahili ni moja katika lugha zinazotumiwa katika maingiliano mengi ya kitaifa. Inasomwa katika viwango mbalimbali vya shule za msingi. Hata hivyo lazima ifahamike kuwa lugha ya Kiswahili inafundishwa katika baadhi ya vyuo vikuu nchini Uganda. Kiswahili pia kinatumika sana jeshini na katika idara ya polisi. Katika Jumuiya ya Afrika Mashariki Kiswahili kimeorodheshwa, kwa mujibu wa itifaki iliyounda jumuiya, kama lugha ya maenezi mapana huku Kiingereza kikihudumu kama lugha rasmi ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (Ripoti ya KAKAMA 2019:1). Lakini mnamo mwaka wa 2016 Kiswahili kimeidhinishwa kama moja katika lugha rasmi na Bunge la Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Kwa sasa Kiswahili kimevuka mipaka ya Bara la Afrika na sasa kinafundishwa katika vyuo mbalimbali katika mataifa ya kigeni kama vile Ujerumani, Uingereza, Marekani, Urusi, Ufina, Ufaransa, Italia, Korea Kusini, Uchina, Oman na kadhalika (Whiteley 1969; Polome 1967; Chiraghdin na Mnyampala 1977; Massamba 2008; Chimerah 1998; Ripoti ya KAKAMA 2019; Niyomugabo 2019). Sudan Kusini ni baadhi ya maeneo ya Afrika ambako Kiswahili kimeenea kwa uchache sana kama anavyodokeza Mazrui (2019: 20):

Bila shaka, hatua ya Sudan Kusini kukubaliwa kujiunga na Jumuiya ya Afrika Mashariki imeleta mkabala mpya wa kiisimu, kwani hii ndiyo nchi ya pekee katika jumuiya hii ambapo Kiswahili hakipatikani kwa haja. Tukio hili halistaajabishi tukizingatia uhusiano ambao umeendelea kwa miaka mingi baina ya nchi za Afrika Mashariki hasa Kenya na Uganda na sehemu hii ya Afrika hata kabla Sudan Kusini haijakuwa nchi huru. Lakini kwa hivi sasa uhusiano baina ya wananchi wa Sudan Kusini na wale wa nchi nyinginezo za Jumuiya unategemea Kiingereza. Je, Kiswahili kitakuwa na nafasi yoyote katika uhusiano huu?

Hali hii ya Kiswahili kuwa nchini Sudan kwa uchache inadokezwa tena na Ripoti ya KAKAMA (2019: 91) ifuatavyo:

Kiwastani imeelezwa kuwa Kiswahili kinatumika katika taifa la Sudan Kusini na watu wapatao milioni mbili hasa katika sekta za benki ambapo habari zimetafsiriwa katika lugha ya

Kiswahili na benki kama vile KCB, Equity Bank na Cooperative. Iielezwa pia kuwa katika benki hizi wenyeji wa Sudan Kusini waliorejea nyumbani huzungumza Kiswahili cha sawa wanapohudumawa. Kiswahili kipo katika sehemu za burudani kama vile katika baa na mikahawa hasa katika miji ya Sudan Kusini.

Licha ya umuhimu wa lugha katika maendeleo ya taifa na ukanda mzima wa Afrika Mashariki, mpaka sasa hakuna utafiti mwingi wa kina ulioangazia suala la Kiswahili nchini Sudan Kusini kwa lengo la kuelewa jinsi kilivyofika huko na hali yake kwa jumla. Hali hii ndiyo ambayo imechochea utafiti huu ili kutaka kuchangia tafiti chache ambazo zimeshughulikia masuala ya Kiswahili nchini Sudan Kusini. Utafiti huu pia ni muhimu kwa sasa kwa kuwa Sudan Kusini ni moja katika nchi za Afrika Mashariki. Wenyeji wake wanapaswa kujua lugha ya Kiswahili na kuitumia kwa mujibu wa Itifaki iliyounda Jumuiya ya Afrika Mashariki. Ili kuweza kushughulikia maendeleo ya Kiswahili kama mataifa mengine ya Afrika Mashariki, taifa la Sudan Kusini pia linapaswa kuunda baraza la Kiswahili. Hali hii ya kutokuwepo kwa Kiswahili cha haja kwa mujibu wa Mazrui (2019) Sudan Kusini inatupa kuuliza kadhaa. Je, taifa la Sudan Kusini litaweza kumudu majukumu ya Kiswahili kwa jinsi gani? Kama kuna Kiswahili kilipata kuingia Sudan Kusini, kiliingia vipi? Ni kwa nini mpaka leo hakuna Kiswahili kingi katika taifa hilo? Ni zipi changamoto zinazokumba lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini kwa sasa? Je ni upi mustakabali wake katika taifa hilo? Haya ni baadhi ya maswali tunayopania kuyajibu katika utafiti huu. Ili kujibu maswali haya tutatumia nadharia ya ujinasibishaji ya Giles (1973) na Giles et al. (1991) ili isaidie katika kueleza namna wenyeji wa Sudan Kusini walivyoweza kukumbatia lugha ya Kiswahili wakati fulani na wakati mwingine kuiacha ili kutumia lugha zao za kienyeji na hata lugha ya maenezi mapana ambayo ni Kiarabu katika mazingira fulani. Kama ambavyo imejadiliwa kwa muda mrefu, kuna sababu mbalimbali zinayofanya makundi au watu binafsi kutumia lugha zingine mbali na lugha wanazozijua. Baadhi ya sababu hizi ni ujuzi wa lugha walionao (Fishman 1965; Platt 1985). Sababu nyingine ni mazingira wanamojipata (Fishman 1965; Galindo 1996; Hammer 2017). Kazi hii kwa kutumia nadharia ya Giles (1973) inataka kubainisha sababu zilizopelekea makundi ya Sudan Kusini kujinasibisha na lugha zinazozungumzwa katika mataifa walikohamia. Je, ilikuwa mapenzi ya hizo lugha ama kulikuwa na sababu zaidi.

Nchi ya Sudan Kusini kijiografia iko katika sehemu ya Afrika Mashariki na kati. Inapakana na nchi za Kenya, Uganda, Ethiopia, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Demokrasia ya Kongo na taifa la Sudan. Sudan Kusini ina makundi mawili ya lugha. Kuna kundi la lugha za kienyeji kama vile Kidinka, Kibari, Kinuer, Kiacholi, Kibaka n.k. Kulingana na Lewis et al. (2016), Sudan Kusini ina takriban lugha za kienyeji 71 na katika lugha hizi, ni lugha 68 ambazo ziko hai kwa maana kwamba bado kuna watu na tamaduni wanaozitumia. Lugha zingine tatu ambazo ni Togo, Mittu na Homa zimo katika hatua za mwisho za kufa na hatimaye kupotea kabisa. Hii ina maana kuwa, lugha hizi za kienyeji hazitumiki tena katika maingiliano na mitagusano ya kawaida na hata katika sherehe, matambiko na shughuli za kiasili: Pia watumiaji wa lugha hizi

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

ambao ni watu wenye umri mpevu sana ni wachache sana sasa hata wanatumia lugha nyinginezo. Hali yao ya uchache na ukosefu wa nguvu za kitamaduni na lugha umesababisha makutano na mwachano na makundi mengine.

Katika kundi la lugha za kienyeji, lugha kubwa ni Kinuer, Kidinka, Kibari na Kizande. Lugha za Sudan Kusini zimo katika makundi makubwa ya kifamilia ya Nilo-Saharan na kundi la Ubangi. Kundi la pili la lugha ni lugha za kigeni kama vile Kingereza, Kiarabu, Kiswahili na Kihispania. Lugha ya Kiingereza inatumika kama lugha rasmi kwa mujibu wa sera ya nchi ya Sudan Kusini. Pia Kiingereza hutumika katika shughuli za kiserikali na pia kama lugha ya kufundishia shuleni. Lugha ya Kiarabu nayo kwa upande mwingine na ambayo ina wasemaji wapatao takriban asilimia 70 inatumika na watu wengi katika mawasiliano mbalimbali kama lugha ya maenezi mapana. Itakumbukwa kwamba Lugha ya Kiarabu cha Sudan Kusini kinatofautiana na Kiarabu cha Misri au Saudi Arabia, kwa mfano.

Methodolojia

Data ya utafiti huu ilikusanywa jijini Nairobi. Tilitumia mfumo wa utafiti nyanjani ambapo tulihoji watu mbalimbali kwa kutumia kifaa cha mahojiano yaliyoratibiwa ili kupata majibu kwa maswali yaliyofungamana na uhamaji kutoka Sudan Kusini na masuala yanayofungamana na matumizi ya Kiswahili. Tulipata kutumia sampuli makundi, sampuli uwezekano na sampuli lengwa. Tuliwahoji sampuli ipatayo watu 22. Katika wahojiwa hawa raia 18 walikuwa kutoka taifa la Sudan Kusini. Tuliwahoji vijana 8; 4 wa kike na 4 wa kiume. Tuliwahoji watu wazima 8. Katika kundi la watu wazima tuliwahoji wanawake 4 na wanaume 4 mtawalia. Katika kundi la watu wazima, tulimhoji afisa mmoja kutoka Ubalizi wa Sudan Kusini jijini Nairobi, Kenya. Tuliimini kuwa balizi huyo angetupa msimamo na maoni ya kutegemewa ya serikali ya Sudan Kusini kuhusu lugha ya Kiswahili nchini humo. Tuliwahoji pia wafanyakazi 4 kila mmoja kutoka Kenya, Uganda, Rwanda na Tanzania mtawalia. Hawa ni watu ambao wanafanya kazi katika mashirika mbalimbali Sudan Kusini. Mwishowe tulihoji wafanyakazi 2 kutoka kambi ya Kakuma. Mahojiano haya yalidumu muda wa dakika ishirini (20) kwa kila mhojiwa. Watu wote tuliwahoji tulipanga kukutana nao ana kwa ana isipokuwa mfanyakazi mmoja wa shirika lisilo la kiserikali kutoka Rwanda tuliyemhoji kwa nja ya simu na wafanyakazi 2 wa kambi ya Kakuma ambao pia tuliwahoji kwa njia ya simu.

Usambaaji wa lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini

Sehemu hii inaangazia nyenzo mbalimbali zilizopelekea kuingia kwa lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini. Nyenzo zinazojadiliwa katika sehemu hii ni vita, biashara, elimu, ndoa na maingiliano ya mipakani. Licha ya kuelezea nyenzo hizo tunajaribu kuonyesha jinsi mfanyiko wa ujinabishaji umesababisha maingiliano ya lugha watu na utamaduni.

Moja katika nyenzo kubwa zilizosaidia kuingia na kuenea kwa lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini ni vita vya wenyewe kwa wenyewe. Vita hivi vilisababisha wakazi wengi wa taifa la Sudan kuhamia katika mataifa jirani kama vile Kenya, Tanzania, Rwanda, Burundi, Eritrea, Ethiopia na Uganda ili kutafuta hifadhi ya kisiasa (Khasandi-Telewa 2007). Mataifa haya ya Afrika Mashariki na eneo la Maziwa Makuu kwa kawaida yanazungumza lugha ya Kiswahili kama lugha ya maenezi mapana (Chimerah 1998; Mazrui na Mazrui 1995). Wakimbizi ambao wengi hawakuwa na kisomo kizuri cha lugha ya Kiingereza walilazimika kukaa na wenyeji ambao waliwasiliana nao kwa kutumia Kiswahili katika mitaa ya chini katika mataifa ya Afrika Mashariki. Katika nchi ya Kenya, kwa mfano, watu wa asili ya Sudan Kusini walikaa katika mitaa kama vile Komarock, Satellite, Kibera na Umoja, Eastleigh miongoni mwa mitaa mingi ya mabanda. Nchini Uganda wakimbizi waliishi katika makazi kama ya Polirinya, Imvepi na Yumbe. Katika kutangamana na wenyeji wa mataifa ya Afrika Mashariki badala ya kujitenga ili kuzungumza lugha za Sudan Kusini, iliwabidi watumie Kiswahili ambayo ni lugha ya kuwanasibisha na wenyeji wao wa mataifa ya Afrika Mashariki. Kwa hali hii basi wenyeji wa Sudan Kusini wakafanya juhudi za kujua lugha ya Kiswahili vizuri ili iwasaidie katika ujinambuzi huu. Lazima tuseme hapa kwamba watu wa Sudan Kusini kama kundi la ndani walitumia lugha za Sudan Kusini kama Kindinka, Kibari, Kinuer n.k. miongoni mwao. Lakini kwa sababu ya wingi wa lugha zao pia ilibidi kutumia Kiswahili hata miongoni mwao na pia walipotaka mawasiliano na watu wengine. Hii ni kwa mujibu ya mahojiano na wenyeji wa Sudan Kusini. Katika hali hii Kiswahili kilikuwa mwafaka zaidi.

Wakimbizi wa Sudan Kusini waliporudi nyumbani baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe katika mwaka wa 2005 na baada ya Uhuru wa taifa lao wa mwaka 2011, walirudi huku wakiwa wajuzi wa lugha ya Kiswahili ambayo kwa ajili ya sababu mbalimbali waliitumia katika miktadha tofauti tofauti. Utapata kwamba katika historia ya Kiswahili si katika Sudan Kusini tu ambako lugha ya Kiswahili ilisambazwa kwa kutumia vita. Hii njia ya kusambaza Kiswahili imekuwapo katika taifa la Uganda pia. Mazrui na Mazrui (1995) kwa mfano, wanaonyesha jinsi vita baina ya Tanzania na Uganda vilisaidia katika kuendeleza na kupenyeza lugha ya Kiswahili katika sehemu mbalimbali za taifa la Uganda, kupitia wanajeshi wa Uganda kuingiliana na wanajeshi wenzao na hata raia wa utawala wa taifa la Uganda wakati wa Idi Amin Dada. Itakumbukwa pia hata Waganda wengi ambao hawakuwa na ujuzi mkubwa wa Kiswahili, nao walikaa nchini Kenya na Tanzania miaka ya sabini na themanini wakati kulipokuwa na vita nchini mwao na kwa njia hii wakajifunza Kiswahili pia hasa pale walipotaka kujinasibisha na wenyeji wao. Itakumbukwa vilevile kwamba pia maingiliano ya wanajeshi wa Tanzania na wanajeshi wa Msumbiji wakati wa vita vya ukombozi vya mataifa ya Kusini mwa Afrika yalisaidia sana katika kusambaza Kiswahili katika maeneo ya Msumbiji, Zimbabwe na hata Afrika Kusini. Kulikuwa na wakimbizi wengi kutoka sehemu za Kusini mwa Afrika waliokaa katika miji mingi ya Tanzania ambako walijifunza Kiswahili na kujinasibisha na wenyeji wa sehemu hizo na kuonyesha umoja nao. Waliporudi nchini Msumbiji, Zimbabwe na Afrika Kusini, walikwenda wakiwa na ujuzi mkubwa wa lugha ya Kiswahili na wakaendelea

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

kuitumia katika maingiliano yao ya kila siku (Chimerah 1998; Mazrui na Mazrui 1995). Hii ndiyo hali iliyotendekeza pia katika nchi ya Sudan Kusini na ikasaidia katika kuingiza lugha ya Kiswahili katika taifa hilo.

Kambi za wakimbizi pia zilikuwa na mchango mkubwa katika usambazaji wa lugha ya Kiswahili kwa wenyeji wa Sudan Kusini na baadaye katika taifa la Sudan Kusini. Ingawa kuna kambi nyinginezo Afrika Mashariki, kama vile Kyangwali nchini Burundi; Nyarugusu, Mtendi na Nduta nchini Tanzania na Imvepi na Yumbe nchini Uganda, tulizingatia sana kambi ya wakimbizi ya Kakuma katika mahojiano ya utafiti huu kwa maana ndiyo kambi iliyokuwa na wakimbizi wengi zaidi kutoka Sudan Kusini. Kwa mujibu wa idara ya wakimbizi nchini Kenya, kambi ya Kakuma imekuwa na takriban wakimbizi laki mbili. Kambi ya Kakuma ilianzishwa kirasmi mnamo mwaka 1992 kwa minajili ya kushughulikia wakimbizi wa Sudan Kusini peke yao (Khasandi-Telewa 2007). Baadaye kwa sababu ya kujaa, kambi zingine kama ile ya Daadab, kuliletwa wakimbizi kutoka Ethiopia, Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo, Burundi, Rwanda, Eritrea, Uganda na Somali na kusababisha kuwepo hata changamoto kubwa zaidi ya lugha ya mawasiliano. Kwa sababu ya watu wengi kutoka sehemu mbalimbali za ulimwengu kukutana katika kambi ya Kakuma na waliozungumza lugha mbalimbali suala la lugha lilikuwa na changamoto kubwa zaidi. Hii ni kwa sababu haya yalikuwa yanazungumza lugha mbalimbali na haikuwa rahisi kujua lugha ya kuidhinisha katika matumizi na ambayo ingekuwa mwafaka kwa kila mtumizi. (Khasandi-Telewa 2007).

Wasimamizi wa kambi ya Kakuma walijaribu sana hata hivyo kuhimiza matumizi ya Kiingereza na Kiswahili hasa shuleni badala ya lugha za kienyeji. Haikuwa rahisi kufundisha kila lugha ya kienyeji katika kambi ya Kakuma. Kwa kutaka kuelewana na makundi mengine wanafunzi kutoka Sudan Kusini wakiwa shuleni basi mbali na kujinasibisha na Kiingereza wakajinasibisha na makundi yaliyozungumza lugha ya Kiswahili. Wafanyakazi wa mashirika mbalimbali, na waaguzi walitumia Kiswahili na Kiingereza walipowasiliana na wakimbizi. Wakimbizi kutoka sehemu za Maziwa Makuu kama vile Rwanda na Burundi wakawa na mazoea ya kutumia Kiswahili; kwa sababu hii basi ilibidi wakimbizi kutoka Sudan Kusini nao kujifunza Kiswahili vilevile ili kujinasibisha na wenzao katika maingiliano yao ya kila siku na wakimbizi wengine kambini. Kwa mujibu ya maoni ya wahojiwa, kwa kiasi kikubwa, iliwabidi wakimbizi wa Sudan Kusini kujifundisha lugha ya wenyeji wao yaani, Kiswahili ili iwe rahisi kwao kupata huduma ya afya, usalama, resheni ya chakula na hata kwa mitagusano ya kawaida na ya kila siku na kuwasilisha malalamiko yao kwa njia iliyo rahisi (Khasandi-Telewa 2007). Kwa mujibu wa Giles (1973) na Giles et al (1991) matumizi ya Kiswahili yaliwawezesha watu wa Sudan Kusini ambao ni kundi la nje kuingiliana vizuri na watu wa sehemu ya Afrika Mashariki ambao ni kundi ndani. Wakimbizi hawa walipoanza kurudi Sudan Kusini mwaka wa 2005, walikuwa na uelewa wa kutosha wa Kiswahili na hivyo kusaidia katika kupeleka Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini.

Elimu pia imekuwa wakala muhimu katika kusambaza na kueneza lugha ya Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini, kulingana na maoni ya wahojiwa kuhusu suala hili. Nchi ya Sudan Kusini itakumbukwa imegawika katika majimbo ishirini na manane. Majimbo mawili ya Sudan Kusini ambayo ni Imatong na Numer Nyang yanapakana na nchi ya Kenya. Wakazi katika majimbo haya mawili wana maingiliano ya kiasi fulani na wenyeji wa taifa la Kenya hasa kielimu. Wanafunzi kutoka majimbo haya ya Sudan Kusini wamekuwa wakitumia mtaala wa Kenya wa Elimu na kutahiniwa na Baraza la Mitihani la kitaifa la Kenya (KNEC) na kwa hivyo kujinasibisha na taasisi za Kenya kielimu na hata kitamaduni. Kwa ajili ya kusoma kwa kutumia mtaala wa Kenya, wanafunzi wa Sudan Kusini wamesoma somo la Kiswahili ambalo ni somo la lazima katika mtaala wa Elimu wa Kenya. Wanafunzi wa Sudan Kusini wamefundishwa na walimu wengi kutoka Kenya na wakawa wana maingiliano kupitia katika Kiingereza na Kiswahili (Kwa Mujibu wa Balozi wa Sudan Kusini nchini Kenya). Katika sehemu hii ya mipakani wenyeji wamelazimika kujinasibisha na majirani zao kutoka Kenya na basi kutumia utamaduni wao wa lugha na pia wa elimu (Giles 1973; Giles et al. 1991). Majimbo haya mawili mpaka sasa ndiyo kitovu kikubwa cha watu wanaojua na kutumia Kiswahili nchini Sudan Kusini. Kulingana na Balozi wa Sudan Kusini tuliyemhoji, endapo taifa la Sudan Kusini litapanga jinsi ya kuendeleza na kuinadi lugha ya Kiswahili, eneo hili la Imatong na Numer Nyang litakuwa muhimu sana kwa mchakato huo. Hii ni kutokana na sababu kwamba watu wa hapa mipakani wanajua Kiswahili cha haja na wanakifurahia. Kwa mujibu wa balozi wa Sudan Kusini tuliyemhoji ni katika sehemu ambako kuna asilimia kubwa ya wasemaji wa Kiswahili.

Wahamiaji wa Sudan Kusini walioenda katika mataifa mbalimbali ya Afrika Mashariki kama katika nchi kama Burundi, Rwanda, Tanzania na Kenya walisajili watoto wao katika shule za nchi hizo za Afrika Mashariki. Katika shule hizi, watoto hawa hali kadhalika walisoma masomo mbalimbali na moja katika masomo ya lazima waliyopaswa kusoma ni somo la lugha ya Kiswahili. Kulingana na wahojiwa hali hii iliwabidi wajifunze sio Kiswahili kwa maingiliano ya kawaida tu na wenyeji wa nchi hizo zilizowahifadhi kama wakimbizi, lakini pia kama somo la kutahiniwa shuleni; hali iliyowafanya kuwa na satua ya juu ya umilisi wa lugha ya Kiswahili. Nchini Kenya, kwa mfano, wanafunzi kutoka Sudan Kusini walitokea kuwa na tajriba kubwa ya Kiswahili kama wanafunzi wa Kenya na sababu kubwa ni kuisoma lugha ya Kiswahili shuleni katika mtaala wa elimu, kwa mujibu wa balozi wa Sudan Kusini nchini Kenya.

Mbali na wakimbizi, kuna kundi la wanafunzi kutoka Sudan Kusini wanaokwenda kutafuta elimu ya juu katika shule za mataifa jirani hasa Uganda, Tanzania na Kenya. Wanafunzi hawa wanalazimika kuingiliana na maeneo wanamosoma na kujifunza Kiswahili vilevile. Wale wanafunzi wanaokuja kujiunga na vyuo vikuu vya Kenya, Uganda Burundi na Rwanda pia hujifunza Kiswahili kama lugha ya maingiliano na watu ya kila siku ili waweze kutagusana na watu mbalimbali katika vyuo wanakosomea masomo yao (Taz Ripoti ya Kakama 2019)

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

Kwa muda mrefu sasa biashara imekuwa nyenzo muhimu ya kusambaza na kueneza lugha ya Kiswahili ulimwenguni (Whiteley 1969; Chimera 1998; Gorman 1974; Mbaabu 1978). Nyenzo hii hali kadhalika imechangia kwa kiasi kikubwa, kuenezwa kwa Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini. Kwanza kabisa majimbo mawili yanayopakana na Kenya ambayo ni Imatong na Nyang licha ya kuhusiana katika elimu kama tulivyotaja hapo huhusiana kibiashara vile vile na watu wa mataifa ya Afrika Mashariki. Lugha ambayo hutumika sana katika biashara hii ya mipakani ni Kiswahili. Wenyeji wa Sudan Kusini ambao taifa lao limetanzwa kisiasa, kiuchumi na kiutamaduni hujinasibisha na upande wa Kenya, Uganda au Tanzania zaidi na katika hali hii kuishia kuifumbata lugha ya Kiswahili zaidi kwa masuala ya biashara mipakani.

Baada ya taifa la Sudan kusitisha vita na Sudan Kusini kupata uhuru, wakazi wa mataifa mengi ya Afrika Mashariki na kati walihamia Sudan Kusini kwa shughuli za kibiashara kama vile biashara za gereji, benki, hoteli, maduka ya rejareja, hospitali, huduma za tekisi, n.k. Watu hawa waliweza kuhamia katika taifa hili kwa sababu ya kuwa na mtaji wa kufanya biashara. Sampuli tuliyoihoji ilikiri kuwa lugha ya Kiswahili katika miji kama vile Juba, Rumbek, Nimule, Wau, Malakal, n.k inatumika kama lugha ya kibiashara. Kwa usemi mwengine watu wengi hujinasibisha na Kiswahili kama lugha ya kibiashara. Katika hali hii basi biashara inasaidia katika kuisambaza na kuisukuma mbele lugha ya Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini japo kwa uchache. Licha ya wafanyakazi hawa kuna wafanyakazi wengi wa mashirika yasiyo ya kiserikali na mashirika mengine ya kutoa misaada. Hawa pia nao wamepeleka lugha ya Kiswahili Sudan Kusini na huitumia katika shughuli zao. Wahamiaji hawa wamekuwa nyenzo muhimu iliyopeleka Kiswahili kuingia nchini Sudan Kusini. Kwa mujibu ya mahojiano na wenyeji wa Sudan Kusini, licha ya wao kutumia Kiswahili miongoni mwao hutumia Kiswahili na wakimbizi ambao walirudi nchini Sudan Kusini baada ya vita vya wenyewe kwa wenyewe katika taifa hilo.

Wenyeji wa Sudan Kusini waliohamia katika mataifa jirani na kukaa kwa muda mrefu walioa wachumba kutoka Sudan Kusini. Lakini kuna baadhi yao amabao waliooa wachumba kutoka Kenya, Tanzania, Burundi, Uganda na hata Jamhuri ya Demokrasia ya Kongo iliwabidi kujinasibisha na Kiswahili zaidi kama lugha kuu ya wachumba wao na kulingana sampuli mojawapo tuliyohoji kuna wale waliojaibu kuwafundisha watoto wao lugha za Sudan Kusini. Hata hivyo jaribio hili halikuwafanya watoto wao kufaulu kuzitumia lugha hizi katika mazingira yaliyotumia Kiswahili kama vile mazingira ya Tanzania, kwa mfano. Licha ya ndoa baina ya wenyeji wa Sudan Kusini, familia za wahamiaji kutoka Sudan Kusini zilizokuwa na uwezo wa pesa kutoka kwa wafadhili pia ziliajiri wafanyakazi na wasaidizi wa nyumbani ambao walizungumza lugha ya Kiswahili na watoto waliozaliwa wakalelewa kwa kuzungumza Kiswahili (Ripoti ya KAKAMA 2019). Mathalan anavyosema Galindo (1996) lugha ikawa yazungumzwa kulingana na mazingira na haya mazingira yakawa ya kujinasibisha watoto na walezi wao. Walezi waliokuwa wanatumia Kiswahili wakawa wana mamlaka zaidi katika kuwashauri watoto kwa kutumia Kiswahili. Kwa mujibu wa mahojiano na wenyeji wa Sudan

JOHN HAMU HABWE

Kusini watoto hawa wadogo ambao wengine, kinyume na wazazi wao, lugha yao ya pekee ilikuwa Kiswahili walichangia pakubwa katika mfanyiko mzima wa kusambaza Kiswahili nchini humo.

Katika miaka ya hivi karibuni wakazi wa Sudan Kusini wamependelea kusikiliza nyimbo za Kiswahili kutoka mataifa mengine ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Mara kwa mara kwa sababu ya ujinasibishaji na mshikamano ulioko baina ya mataifa ya Afrika mashariki na Sudan Kusini huwa kuna mialiko ya mara kwa mara ya wanamuziki watumiao Kiswahili kwenda Sudan Kusini kuimba na kuwatumbuiza wenyeji (Ripoti ya KAKAMA 2019: 102). Katika hali hii Kiswahili kinatangazwa, kuenezwa na kupigiwa upatu nchini Sudan Kusini.

Taifa la Sudan Kusini tulivyotaja tayari linapakana na nchi ya Uganda, na vile vile nchi ya Kenya. Kwa muda mrefu kumekuwa na maingiliano ya mipakani ambayo imesaidia kuingiza lugha ya Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini (Ripoti ya Kakama 2019). Wakazi wa Sudan Kusini wanapokwenda nchini Kenya au Uganda kwa ajili ya huduma mbalimbali hupata kutangamana na watumizi wa lugha ya Kiswahili na mitagusano hii aghalabu hutumia lugha ya Kiswahili kama lugha ya maenezi mapana. Nchi ya Uganda inapakana na Sudan Kusini na watu wa Sudan Kusini hutumia Kiswahili kwa kiasi fulani katika maingiliano yao na watu kutoka Uganda. Pia kuna maingiliano makubwa baina ya wakazi wa majimbo ya Imatong na Numer Nyang na watu kutoka Kenya. Lugha inayotumika licha ya Kiingereza ni Kiswahili. Hali hii husababishwa na haja kubwa ya kujinasibisha kwa upande wa makundi ya kutoka Sudan Kusini. Unajibishaji huu hujikita kwenye upevu wa kiutamaduni na maendeleo ya kiuchumi yanayodhihirishwa na makundi ya Kenya na Uganda. Katika maingiliano ya mipakani, licha ya elimu maingiliano ya kibiashara na kiuchumi hutokea. Kwa mujibu wa Ripoti ya KAKAMA (2019:95) matumizi ya lugha ya Kiswahili katika sehemu za mipakani yanadhihirika japo kwa uchache miongoni mwa wakazi, taasisi za kiafya na kambi za kijeshi.

Harakati za Jumuiya ya Afrika Mashariki bila shaka zitakuwa na athari kubwa katika maendeleo ya Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini. Kutakuwa na maingiliano mengi miongoni mwa watu wa mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Watu wa kutoka mataifa mengine ya Jumuiya ya Afrika Mashariki tayari wanasafiri hadi Sudan Kusini ili kushughulika na mambo mbalimbali ya kiuchumi hususan ya kibiashara. Watu wa Sudan Kusini nao wanasafiri na kwenda katika nchi mbalimbali za Jumuiya ya Afrika Mashariki kutafuta elimu na mahusiano ya kiuchumi. Kuna wakazi wa Sudan Kusini wanaotembelea mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutafuta fursa ya kukeza. Kuna pia wenyeji wa Sudan Kusini wanaokaa katika mataifa mengine ya Afrika Mashariki kwa shughuli za kibiashara na kazi zingine kama vile wafanyakazi wa balozi mbalimbali. Lugha wanayotumia, kwa mujibu wa mahojiano, hasa katika mitagusano ya moja kwa moja na watu wa kawaida ni Kiswahili. Hali hii inaendelea kueneza lugha ya Kiswahili katika taifa la Sudan Kusini. Maana wenyeji wa Sudan Kusini wanazidi kuijua lugha ya Kiswahili kwa ajili ya maingiliano yanoyosababishwa na kutaka kujinasibisha na watu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki zaidi.

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

Kwa muda mrefu sasa dini imekuwa na nafasi kubwa katika kuendeleza lugha ya Kiswahili (Whiteley 1969; Mazrui na Mazrui 1995). Dini ambayo imechangia kukua kwa Kiswahili ni dini ya Kiislamu. Lakini dini ya Kikristo pia imekuwa na mchango adhimu katika jukumu hilo. Wakimbizi wa Sudan Kusini walijiunga na makanisa na miskiti katika mataifa mbalimbali ya Afrika Mashariki. Huko katika masuala ya kuabudu walikuwa ni kundi dogo ikabidi wajinasibishe na wengi na wengi wale walitumia Kiswahili katika miskiti na makanisa. Hata katika kambi nyingi masuala ya dini yaliendeshwa kwa Kiingereza pamoja na Kiswahili. Kuna vikundi fulani vilivyoanzisha makanisa yao maalum kwa watu wa Sudan Kusini na wakawa wanatumia Biblia, vitabu vya nyimbo vilivyoandikwa katika lugha kuu za Sudan Kusini kama vile Kidinka. Hata hivyo mjumuiko wa wenyeji Sudan Kusini kutoka makabila mengine na kuwepo na watoto wasiojua lugha za kienyeji za Sudan ukawafanya kutumia Kiingereza na Kiswahili. Mtagusano wa kidini umesaidia kwa kiasi fulani japo kidogo kusambaza Kiswahili (Mazrui na Mazrui 1995)

Lazima tuseme hapa kuwa mfanyiko wa ujinasibishaji uliowafanya watu wa Sudan Kusini kutaka kujua Kiswahili umezaa makundi ya aina mbili ya wasemaji wa Kiswahili. Kuna kundi la kwanza ambalo ni la watu walioingiana na utamaduni wa lugha ya Kiswahili na wakajifunza lugha hii kwa upevu mkubwa. Waliidhibiti lugha katia viwango vya fonolojia, mofolojia, sintakisia na semantiki yake. Hili ni kundi linalojumlisha wanafunzi wanaosoma katika shule za Tanzania, Kenya, Burundi na Rwanda. Kundi hili lina satua ya juu ya Kiswahili. Lakini kundi la pili ni lile ambalo limejinasibisha lakini halikupata kumudu Kiswahili kwa kiwango kikubwa. Linatumia Kiswahili lakini chenye athari kubwa ya lugha za Sudan Kusini. Athari hizi kwa mujibu wa wahojiwa zinadhahirika katika sana katika fonolojia, mofolojia na sintakisia au hata semantiki ya usemi wao na matumizi. Hili ni kundi ambalo limekuwa tofauti kidogo na kundi la kwanza lililo na umilisi mkubwa wa Kiswahili.

Changamoto na mustakabali wa Kiswahili nchini Sudan Kusini

Licha ya Kiswahili kupenya katika taifa la Sudan Kusini, kuna changamoto kadhaa zinazoweza kuikabili lugha hii nchini humo. Changamoto mojawapo ya maenezi ya Kiswahili nchini Sudan Kusini ni ile ya kutokuwa na vyombo mahsusi vya dola vya kiseru ambavyo vitakifanya Kiswahili kibaki hai na hata kukubalika na watu wengi. Ni kweli kuwa kuna mpango wa kukipa Kiswahili nafasi ya lugha ya maenezi mapana katika taifa la Sudan Kusini. Lakini hili nalo pekee halitoshi; lazima kuwepo na taratibu maalum za kuiendeleza na kuinadi lugha ya Kiswahili ili watu waikubali na kuenzi.

Changamoto nyingine ni kuwa, itabidi taifa la Sudan Kusini kufanya juhudi kubwa za kurejesha amani ya kudumu na utangamano katika taifa lao. Juhudi hii si kidogo. Sudan itahitaji msaada wa mataifa jirani ili kufaulisha jambo hili. Amani ya kudumu ikirudi basi na mipango

ya lugha na hata kutekelezwa kulingana na sera ya serikali itakuwa rahisi. Bila Amani kuwepo Sudan Kusini mipango ya lugha haitaweza kufaulu.

Bila shaka kuna changamoto ya kukua kwa Kiswahili inayotokana na lugha za kienyeji kama vile Kidinka, Kinuer, Kibari na Kizande. Katika muktadha huu ni wazi kuwa lugha ya Kiswahili na wasemaji wake watakuwa kundi la nje kwa mujibu wa mtazamo wa Giles (1973; Giles 1980, Giles na Powesland 1975). Hali hii italeta mashindano makubwa baina ya hili kundi la nje la Kiswahili na makundi ya ndani ya kienyeji. Kutatokea haja kubwa ya kutaka kuwa na mwachano wa kilugha. Wenyeji watataka lugha zao ziendelezwe hasa wenyeji wa makundi makubwa yaliyo na ushawishi mkubwa wa kisiasa na kijamii kama vile Wanuer na Wadinka. Makundi haya makubwa ndiyo yanayong'ang'ania uongozi wa kisiasa wa kitaifa kwa sasa katika taifa la Sudan Kusini na kuna uwezekano mkubwa kila moja katika makabila haya kila kundi litataka kuwa na ushawishi mkubwa. Chombo kimojawapo cha kudhibiti taifa ni kutumia lugha. Hali hii inafanana na jinsi kundi fulani la Waganda lilivyoziua kuenea kwa Kiswahili nchini Uganda na kutaka lugha ya Kiganda itumike kote nchini. Kupitia Daudi Kabaka, walimwandikia Gavana W.F Gowers kusema hawakutaka Kiswahili kutumika nchini Uganda (Whiteley 1968; Mazrui na Mazrui 1995; Chimera 2000).

Kuna uwezekano mkubwa pia wa lugha ya Kiswahili inaweza kutazamwa kama lugha ya kigeni, hali ambayo inaweza kudumaza kakubalika na kuendelezwa kwake na kufanya baadhi ya wakazi wa Sudan Kusini kutojinasibisha nayo. Isitoshe, mfungamano wa Kiswahili na dini ya Kislamu ni suala linaloweza kufanya wenyeji wa Sudan Kusini kutoionea fahari na hata kuikubali. Itakumbuka moja katika sababu zilizofanya baadhi ya wenyeji wa Demokrasia ya Kongo kupinga Kiswahili lilikuwa ni suala la Kiswahili kufungamana na Uislamu. Na hali hii inaweza kuwa tishio kubwa nchini Sudan Kusini kuliko hata taifa la Demokrasia la Kongo. Wengi tuliowahoji wameona Kiswahili kinahalalisha Uislamu, kipengele ambacho kimewafanya kuuvunja uhusiano wao na Sudan, ambako wakazi wake wengi ni Waislamu na Waarabu.

Lugha ya Kiingereza bado itapewa nafasi kubwa na kwa hivyo kuwa na ujasibishaji mwingi na watu kuliko Kiswahili. Katika juhudi zozote za kuendeleza lugha nchini Sudan Kusini Kiingereza ni tishio la wazi, la upanukaji na usambaaji wa lugha ya Kiswahili. Watu wengi kutoka Sudan Kusini wanachangamkia na kujinasibisha zaidi na lugha ya Kiingereza kwa sababu imefungamana na ubora wa maisha na maendeleo ya kimataifa na huenda ikaziua Kiswahili kuingia kikamilifu na kukita mizizi. Kiswahili kinapaswa kuchukua nafasi ya Kiarabu kwa mujibu wa balozi wa Sudan Kusini nchini Kenya. Itachukua muda mrefu kwa sababu kwa sasa watu wengi waliosoma wanazumgumza Kiarabu hasa Kiarabu kisicho rasmi yaani Kiarabu cha mitaani. Mustakabali wa Kiswahili utategemea sera ya lugha nchini Sudan Kusini kulemaza maendeleo ya Kiswahili katika kukubaliwa na kunadiwa.

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

Hitimisho

Utafiti huu ulilenga kuchunguza maenezi ya lugha ya Kiswahili nchini Sudan Kusini kwa kuzingatia nyenzo zilizosaidia katika kuisambaza, na baadhi ya changamoto za lugha hii nchini humo na mustakabali wake utafiti umeonyesha kuwa lugha ya Kiswahili imeingia Sudan Kusini kwa kupitia vita vilivyosababisha wakazi kuhama na kwenda katika mataifa ya Afrika Mashariki wanakozungumza Kiswahili. Licha ya vita, wafanyabiashara kutoka mataifa jirani wanaohamia Sudan Kusini wamesaidia katika kupeleka Kiswahili nchini Sudan Kusini na kukisambaza hata zaidi katika shughuli zao za kazi. Mbali na vita na biashara, nyenzo nyingine muhimu ambazo zimechangia kuingia Kiswahili katika Sudan Kusini ni elimu, mitagusano ya mipakani na mahusiano kama vile ndoa kati ya wakazi wa Sudan Kusini na wenyeji wao kutoka nchi kama vile Uganda, Tanzania na Kenya. Kwa kutumia mtazamo wa Giles wa ujinasibishaji utafiti umeonyesha kwamba hata kama wakimbizi kutoka Sudan walikuwa na lugha zao walilazimika kujinasibisha na makundi walikohamia kitamaduni na kilugha, hivyo basi wakalazimika kujua Kiswahili.

Utafiti umeonyesha hali ya lugha na nafasi ya Kiswahili ambayo ni ndogo mno kwa sasa katika taifa la Sudan Kusini. Utafiti huu umebaini kuwa hata kama Kiswahili kimeingia Sudan Kusini, kuna changamoto si haba za kukiendeleza kutokana na lugha za kienyeji kuwa tishio na lugha nyingine za maenezi mapana kama vile Kiarabu na Kiingereza. Hata hivyo kwa sababu ya juhudi za Jumuiya ya Afrika Mashariki Kiswahili kina nafasi kubwa ya kuingia katika taifa la Sudan Kusini na kukubaliwa na baadaye kushamiri humo nchini kama ilivyo katika mataifa mengine ya Afrika Mashariki.

Marejeleo

- Chimerah, Rocha 1998. *Kiswahili, Past Present and Future*, Nairobi: University of Nairobi.
- Chiraghdin, Shihabuddin na Mnyampala, Mathias. 1977. *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Oxford University Press.
- Fishman, Joshua. 1965. Who speaks what language and to whom? *La Linguistique* 1(2): 67-88.
- Galindo, Leticia 1996. Language use and language attitudes: A study of border women. *Bilingual Review La Revista Bilingüe* 2(1): 5-17.
- Giles, Howard. 1973. Accent mobility: A model and some data. *Anthropological Linguistics* 15: 87-109.
- Giles Howard 1980. Accommodation theory: Some new directions. Katika de Silva (mh) *Aspects of Linguistic Behaviour*. uk. 105-136. York, England: York University Press.

- Giles, Howard. na Powesland, Peter 1975. *Speech Styles and Social Evaluation*. London: Academic Press.
- Giles, Howard et al. 1991. Accommodation theory: communication, context and consequence. Katika H. Giles et al. (wah), *Contexts of Accommodation. Development in Applied Sociolinguistics*. uk. 1-68. Cambridge: Cambridge University Press.
- Gorman, Tommy 1974. The Development of Language Policy in Kenya with Particular Reference to the Educational Systems. Katika Whiteley, W. H. (Mh), *Language in Kenya*. Nairobi: Oxford University Press: 397-446.
- Hammer, Kates 2017. They Speak What Language and to Whom?! A Culturation and Language Use for Communication. *Language and Communication* 56: 42-54.
- Khasandi-Telewa, Vicky 2007. *English is a Must to Us: Language and Education in Kakuma Refugee Camp, Kenya*. Unpublished PhD Thesis, University Warwick.
- Lewis, Paul. et al. (Wah). 2016. *Ethnologue; Languages of the World* (Nineteenth ed.). Texas: SIL International.
- Massamba, David. 2008. *Historia ya Kiswahili*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- Mazrui, Ali. & Mazrui, Al- Almin 1995. *Swahili State and Society*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Mazrui, Al-Almin. (2019). Kiswahili katika mwelekeo wa Afrika Mashariki. Katika Ken Walibora et al. (Wah) *Kiswahili Utangamano na Maendeleo Endelevu Afrika Mashariki*. Zanzibar: KAKAMA: 16-30.
- Mbaabu, Ireri. 1978. *Kiswahili Lugha ya Taifa*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Niyomugabo, Charles (2019). Kiswahili nchini Rwanda: ufunguo wa maendeleo endelevu. Katika Ken Walibora et al. (Wah), *Kiswahili, Utangamano na Mendeleo Endelevu Afrika Mashariki*. Zanzibar: KAKAMA: 68-79.
- Platt, John. 1985. Social class ethnicity and language choice: language use in major shopping areas in Singapore. *Southeast Asian Journal of Science* 13(1): 61-81.
- Polome, Edgar 1967. *Swahili Handbook*. Washington D. C.: Centre for Applied Linguistics.
- Ripoti ya KAKAMA 2019. *Capacity Assessment of the Development and Use of Kiswahili in the EAC*. Zanzibar.

KISWAHILI NCHINI SUDAN KUSINI

Senkoro, Mbazi 2019. Kiswahili Afrika: Jana Leo na Kesho katika Ken Walibora (Wah), *Kiswahili Utangamano na Maendeleo Endelevu Afrika Mashariki*. Zanzibar: KAKAMA.

Whiteley, Howard. 1969. *The Rise of a National Language*. London: Methuen.